


Bibilia ya watoto
Inawalettea

Msamaria Mwema



Kimeandikwa na: Edward Hughes
Kimeorodheshwa na: M. Maillot; Lazarus
Imerekebishwa na: Ruth Klassen; Sarah S.

Alastair Paterson

Kimetafsiriwa na: Bethel Children's Home,
Kisumu, Kenya and Emmanuel Menya
Kimedhibitishwa na: Bible for Children
www.M1914.org



BFC
PO Box 3
Winnipeg, MB R3C 2G1
Canada

©2020 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii, lakini bila ya kuuza.



"Mwalimu, nifanye nini ili
nipokee uzima wa milele?"
Mtu aliyeuliza hili swali
alikuwa ni mwanasheria,
akitaka
kumjaribu
Yesu.



Yesu akamjibu "Sheria
ya Mungu inasemaje?"



Huyu mtu akasema,
"Mpende Mungu na jirani
yako." Akauliza, "Lakini
jirani yangu ni nani?"




Ili kujibu swali la huyu mtu, Yesu akasimulia hadithi ya mtu aliyekuwa anasafiri kutoka Yerusalemu kwenda Yeriko. Huyu mtu alivamiwa na wanyang'anyi.



Wanyang'anyi waliiba kila kitu walichoweza kupata,
hata wakavua nguo za huyu mtu mwenye bahati
mbaya na kuzichukua. Pia walimjeruhi vibaya
sana, wakamuacha karibu ya
kufa kando ya

barabara.



Kwa bahati kuhani mmoja akashuka
kwa njia ile. Kwa hakika angemsaidia
huyu mtu aliyejeruhiwa.

Hakufanya
hivyo!

Alipomuona
huyu

mtu akivuja damu,
akapita kando upande mwingine wa barabara.



Mara sauti ya uwayo wa mguu ikaashiria kwamba
mtu mwingine anakaribia mahali hapo. Alikuwa
Mlawi - mtu aliyewasaidia makuhani hekaluni.
Alisogea na kumtazama huyu mtu
aliyeumizwa, kisha



akaondoka zake bila kutoa msaada.



Hatimaye Msamaria akafika. Wayahudi
waliwachukia Wasamaria. Watu
waliokuwa wanasikiliza hadithi ya
Yesu hawakutarajia Msamaria


awe ndiye
shujaa.




Lakini alikuwa ndiye shujaa. Msamaria alijali, na akasimama ili kusaidia.



Msamaria alipiga magoti,
akaweka dawa polepole
na kufunga majeraha ya
huyu mtu asiyemjua.
Kisha akamsaidia huyu
mtu aliyemizwa kupanda
juu ya punda wake
mwenyewe.




Kwenye nyumba ya wageni kando ya barabara, Msamaria akamhudumia huyu mtu usiku wote.



Asubuhi akamlipa mwenye nyumba
ya wageni ili amtunze huyo msafiri
mpaka apone.



Hadithi ikafikia mwisho. Yesu akauliza,
"Nani alikuwa jirani yake yule mtu
aliyeumizwa?"






Mwanasheria
akajibu, "Jirani
yake alikuwa ni
Msamaria
aliyemuonea
huruma."



Yesu akamwambia, "Enenda zako, nawe ukafanye vivyo hivyo." Jirani ni mtu yeyote mwenye hitaji. Tunaweza kuonyesha upendo kwa kuwasaidia watu wenye mahitaji. Hilo linampendeza Mungu.



Msamaria Mwema

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Luka 10

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."


Zaburi 119:130





Mwisho

46



60



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

